MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA

# MFUKO WA ELIMU

Jarida la Saba la Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

www.tea.or.tz Julai - Oktoba 2025

## TEA, KOICA NA UNICEF WASHIRIKIANA MIRADI YA STEM








- TEA IKO TAYARI KUTEKELEZA MIRADI YA AMALI. UK. 2
- TEA NA TAHA WAJADILI USHIRIKIANO. UK. 9


*"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"*

# KUHUSU TEA

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)** ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya 2001 chini ya kifungu cha 5 (1) ili kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu, ulioanzishwa kwa sheria hiyo hiyo. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

Madhumuni ya Mfuko wa Elimu ni kuongeza nguvu za Serikali katika kugharimia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa, katika ngazi zote za Elimu kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.



## DIRA

Kuwa Mfuko wa Elimu bora wenye hadhi ya kimataifa unao tatua changamoto za elimu nchini, kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya mapato katika kuchangia maendeleo endelevu nchini.



## DHAMIRA

Kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuzigawa rasilimali hizo kwa ufanisi katika kufadhili miradi ya elimu ili kuboresha upatikanaji wa elimu bora na ujuzi kwa usawa.

# YALIYOMO

SALAAM ZA MKURUGENZI MKUU....iii

TEA, KOICA NA UNICEF WASHIRIKIANA KATIKA MIRADI YA STEM: KUNUFAISHA ZAIDI YA WANAFUNZI ELFU 10............01

TEA IKO TAYARI KUTEKELEZA MIRADI YA AMALI....02

MWALIMU MISENYI AOMBA MAABARA ZA SAYANSI NA MAJENGO YA UTAWALA....03

HABARI KATIKA PICHA....04

AFISA ELIMU SEKONDARI LIWALE AOMBA UFADHILI WA MABWENI YA WASICHANA ....06

TEA YAFANYA ZIARA YA KIKAZI KATIKA OFISI ZA UNICEF ZANZIBAR KUIMARISHA USHIRIKIANO....07

WFP KUSHIRIKIANA NA TEA KATIKA MPANGO WA CHAKULA SHULENI....08

TEA NA TAHA WAJADILI USHIRIKIANO....09

# TIMU YA UHARIRI

**Mwenyekiti:** Masozi Nyirenda

**Mhariri:** Bestina Magutu

**Wachangiaji:** Eliafile Solla

Joyce Minja

# ANUANI:

**Mamlaka ya Elimu Tanzania(TEA)**

**S. L.P 2516, Dodoma- Tanzania**

**Barua pepe: info@tea.or.tz,**

**Tovuti www.tea.or.tz,**

**Instagram: Officialteatz,**

# SALAMU ZA MKURUGENZI MKUU



Karibu kwenye toleo hili maalumu la Jarida la Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), linaloangazia juhudi, mafanikio na ushirikiano mbalimbali unaochochea maboresho ya miundombinu na ubora wa elimu nchini. Kupitia toleo hili la saba, tunakuletea taarifa mahsusi kuhusu miradi inayotekelezwa na TEA kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, taasisi za serikali, na wanufaika kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Katika kipindi hiki, TEA imeendelea kusimamia na kuratibu miradi mikubwa ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, hususan katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), mafunzo ya amali, na miradi ya elimu jumuishi inayolenga kuongeza upatikanaji wa elimu bora na salama kwa watoto na vijana.

Kupitia ushirikiano na KOICA na UNICEF, TEA inaanza kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa maabara za sayansi na TEHAMA katika shule 13 za sekondari mikoa ya Dodoma na Simiyu. Mradi huu wenye thamani ya takribani shilingi bilioni sita unatarajiwa kufungua fursa pana kwa zaidi ya walimu na wanafunzi 10,400.

Katika kuimarisha elimu ya amali, Mamlaka ya Elimu Tanzania(TEA) inaendelea kupanua wigo wa miradi mbalimbali inayolenga kuweka mazingira wezeshi ya kujifunzia stadi mbalimbali ikiwa pamoja na kilimo, michezo na fani nyingine za kitaalamu. Uongozi wa TEA umeendelea kukutana na wadau muhimu katika sekta ya elimu na maendeleo, wakiwemo Shirika la Chakula Duniani (WFP), Chama cha Wakulima wa Mazao ya Bustani Tanzania (TAHA), na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya ufadhili, lishe shuleni, teknolojia safi za kupikia, na mafunzo ya vijana.

Aidha, shule kutoka maeneo mbalimbali zimeendelea kufaidika na ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa ambapo maboresho ya miundombinu, upatikanaji wa vifaa, na programu za mafunzo vimeendelea kubadilisha mazingira ya elimu kwa manufaa ya walimu, wanafunzi na jamii.

Jarida hili pia linamulika maoni na maombi ya wadau waliotembelea banda la TEA katika Maonyesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara (Saba Saba), ikiwemo haja ya maabara za sayansi, majengo ya utawala, mabweni ya wasichana na nyumba za walimu mahitaji ambayo TEA inaendelea kuyafanyia kazi kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali.

Tunakuomba uendelee kufuatilia taarifa hizi muhimu zinazoonyesha dhamira ya TEA katika kuendeleza ubora wa elimu nchini, kwa ushirikiano na wadau mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.

**Dkt. Erasmus F. Kipesha**
*Mkurugenzi Mkuu-TEA*

# 1. TEA, KOICA NA UNICEF WASHIRIKIANA MIRADI YA STEM: KUNUFAISHA ZAIDI YA WANAFUNZI ELFU 10

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) wanatekeleza kwa pamoja mradi wa kuweka miundombinu wezeshi kwa ajili ya masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), wenye thamani ya Takribani Shilingi bilioni sita.

Mradi huo unahusisha ujenzi wa maabara tatu za sayansi na moja ya TEHAMA katika kila shule za sekondari 13 zinazonufaika na mradi huo katika mikoa ya Dodoma na Simiyu, ambapo jumla ya maabara 52 zinatarajiwa kujengwa, na hivyo kunufaisha walimu na wanafunzi zaidi ya 10,400.

Utekelezaji wa mradi huu umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2025/2026 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2026.

Katika maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo, Menejimenti ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ilikutana na wawakilishi wa KOICA na UNICEF tarehe 8 Septemba 2025. Katika kikao hicho, TEA ilieleza namna inavyotekeleza miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, ambao inausimamia.

Mkutano huo, ulioongozwa na Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, CPA Mwanahamis Chambega, ulijumuisha mawasilisho kuhusu majukumu ya TEA na utekelezaji wa miradi ya elimu inayoendeshwa na Mfuko wa Elimu wa Taifa.

Mratibu wa mradi huo wa STEM kwa upande wa TEA, Bw. Halfan Magani, alihakikishia wadau kuwa TEA itasimamia utekelezaji wa mradi huo kwa ufanisi ili kuhakikisha ubora na ukamilishaji kwa wakati.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, TEA kwa kushirikiana na UNICEF ilitekeleza miradi 13 yenye thamani ya Shilingi milioni 854. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, miradi 35 yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.55 ilitekelezwa, ikihusisha ujenzi na ukarabati wa maabara za sayansi, vyumba vya madarasa, na matundu ya vyoo katika mikoa ya Tabora, Songwe, na Kigoma.




*Wajumbe wa Mkutano wa pamoja baina ya TEA, UNICEF na KOICA*

# 2. TEA IKO TAYARI KUTEKELEZA MIRADI YA AMALI

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Dkt. Leonard Akwilapo, amesema Mamlaka imejipanga kutekeleza miradi inayolenga kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya mafunzo ya amali nchini.

*“Sisi kama Mamlaka ya Elimu Tanzania, tumepewa fedha za kutosha kutekeleza miradi ya mafunzo ya amali katika shule zilizoteuliwa kutoa mafunzo hayo,”* amesema Dkt. Akwilapo.

Akizungumza baada ya kutembelea banda la TEA katika Maonyesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara (Saba Saba) jijini Dar es Salaam, Dkt. Akwilapo alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha zinazowezesha TEA kutekeleza miradi kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa.

Ameongeza kuwa TEA itaendelea kufadhili miradi ya kuimarisha miundombinu ya kufundishia mafunzo ya amali katika shule za sekondari na vyuo.
.

Aidha, ameeleza kuhusu utekelezaji wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF), unaosimamiwa pia na TEA, ambapo zaidi ya vijana 49 wamepata mafunzo yanayowawezesha kujipatia kipato

Akiwa katika banda la TEA, Dkt. Akwilapo alizungumza na baadhi ya wanufaika wa mafunzo hayo waliopata ufadhili kupitia SDF.

TEA imeshiriki Maonyesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara kwa lengo la kutoa elimu na kukutana na wadau muhimu ili kuimarisha mahusiano ya kikazi.

Katika mwaka wa fedha 2025/2026, TEA inaendelea kutekeleza miradi ya mafunzo ya amali katika shule 20 za sekodari kote nchini yenye thamani ya Shilingi bilioni 3 ikihusisha mafunzo katika nyanja za kilimo, michezo, na maeneo mengine ya kitaalamu.




*Mwenyekiti wa Bodi ya TEA Dkt. Leonard Akwilapo akifurahia bidhaa na tuzo za mmoja wa wanufaika wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi Bi. Ester Shebe (kulia) alipotembelea banda la TEA wakati wa maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa, maarufu Sabasaba.*

# 3. MWALIMU MISENYI AOMBA MAABARA ZA SAYANSI NA MAJENGO YA UTAWALA

Mwalimu Gotfrid Michael wa Shule ya Sekondari Gwajae, Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera, amepongeza huduma zinazotolewa kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, akisema zimekuwa muhimu katika kuboresha miundombinu ya elimu hasa katika maeneo yaliyoko pembezoni.

Akizungumza katika banda la TEA wakati wa Maonyesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara (Saba Saba) jijini Dar es Salaam, Mwalimu Michael alieleza changamoto ya uhaba wa majengo ya utawala katika shule za Halmashauri ya Misenyi, hali inayowalazimu walimu kutumia vyumba vya madarasa kama ofisi.

Ametaja changamoto nyingine kuwa ni uhaba wa maabara za masomo ya sayansi, jambo linalokwamisha ufanisi katika ufundishaji wa masomo hayo.

Aidha, amesema katika shule yake ya Gwajae kuna upungufu mkubwa wa nyumba za walimu, hivyo walimu wanalazimika kutembea umbali mrefu kila siku kutoka makazi yao hadi shuleni. Ameomba TEA kusaidia ujenzi wa nyumba za walimu ili kuboresha mazingira ya kufundishia.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, TEA imetekeleza jumla ya miradi mitano katika mkoa wa Kagera, yenye thamani ya takribani Shilingi milioni 466 ikihusisha ujenzi wa nyumba za walimu, jengo la utawala pamoja na usambazaji vifaa vya TEHAMA katika shule za Katale Sekondari, Katale Shule ya Msingi, Maruku Sekondari,Bukare Sekondari na Nyakato Sekondari.




*Mwalimu Gotfrid Michael kutoka Shule ya Sekondari Gwajae iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)*

# 4. HABARI KATIKA PICHA




*Timu ya TEA iliyoshiriki katika Maonyesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Saba Saba*




*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Suleiman Serera (kushoto) akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi CPA. Mwanahamisi Chambega*

# 5. HABARI KATIKA PICHA



Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) Dkt Aneth Komba akipokea zawadi alipotembelea banda la TEA



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Dkt. Leonard Akwilapo akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TEA






Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi CPA. Mwanahamisi Chambega akiwahudumia wageni waliotembelea banda la TEA




Wadau wakipata elimu kuhusu Mamlaka ya Elimu Tanzania

# 6. AFISA ELIMU SEKONDARI LIWALE AOMBA UFADHILI WA MABWENI YA WASICHANA

Afisa Elimu wa Idara ya Elimu Sekondari, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Bi. Kajhui Bofu, amesema Mfuko wa Elimu unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) umeleta manufaa makubwa katika sekta ya elimu kutokana na kuboresha miundombinu ya elimu nchini.

Akizungumza katika banda la TEA wakati wa Maonyesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara (Saba Saba) 2025, Bi. Bofu alieleza kuwa Mfuko wa Elimu wa Taifa umeendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo, na kutoa wito kwa wadau wa elimu kuendelea kuchangia mfuko huo kwani fedha hizo huwafikia walengwa.

Ametoa mfano kuwa wakati akiwa Afisa Elimu Vifaa na Takwimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Mfuko huo ulifadhili ujenzi wa nyumba za walimu katika Shule ya Sekondari Kandawale (Six-in-One houses) yenye uwezo wa kutoa makazi kwa familia sita za walimu pamoja na jengo la utawala katika Shule ya Sekondari Namayuni.

Ametumia fursa hiyo kuomba ufadhili wa ujenzi wa mabweni mawili kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Namaghoa, akisema hatua hiyo itakuwa na manufaa makubwa kwani wanafunzi wa shule hiyo wamekuwa wakifanya vizuri katika mitihani yao.

Aidha, amesema ujenzi wa mabweni hayo utawezesha shule hiyo kuanzisha masomo ya kidato cha tano na sita.



*Bi. Kajhui Bofu Afisa Elimu Idara ya Elimu Sekondari, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale mkoani Lind akipata elimu zaidi kuhusu Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).*

# 7. TEA YAFANYA ZIARA YA KIKAZI KATIKA OFISI ZA UNICEF ZANZIBAR

Katika jitihada za kuimarisha uhusiano na wadau wa maendeleo, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) imefanya ziara ya kikazi katika Ofisi za Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Zanzibar tarehe 12 Agosti 2025.

Lengo la ziara hiyo lilikuwa kujitambulisha na kujadili namna ya kuendeleza ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya elimu nchini.

Ujumbe wa TEA uliongozwa na Bw. Masozi Nyirenda, Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi, akiambatana na Bi. Prisca Kalungura, Mtaalamu wa Usanifu wa Majengo, na Bw. Saidi Bungara, Mhandisi wa Ujenzi.

Walikutana na Mkuu wa Ofisi ya UNICEF Zanzibar, Dkt. Laxmi Majji, pamoja na Dkt. Masoud Salim, Mtaalamu wa Elimu wa UNICEF Zanzibar. Mazungumzo yalilenga kuimarisha ushirikiano katika nyanja za ufadhili na utekelezaji wa miradi ya elimu Tanzania Bara na Zanzibar, ili kuhakikisha watoto wote wanapata elimu bora na salama.



*Ujumbe Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ukiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi Bw. Masozi Nyirenda pamoja na ujumbe wa UNICEF Zanzibar wakiwa katika ofisi za UNICEF – Zanzibar*

# 8. WFP KUSHIRIKIANA NA TEA KATIKA MPANGO WA CHAKULA SHULENI

Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) limeeleza dhamira yake ya kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) katika kutekeleza mpango wa chakula mashuleni unaolenga kuwapatia wanafunzi lishe bora wakiwa shuleni.

Mpango huu utasaidia kuongeza mahudhurio, umakini darasani, ufaulu na afya bora miongoni mwa wanafunzi, hivyo kuchochea maendeleo ya elimu.

Dhamira hiyo ilielezwa tarehe 31 Julai 2025 katika mkutano wa wadau wa elimu uliojadili matumizi ya nishati safi ya kupikia (E-Cooking) mashuleni. Teknolojia hii itawezesha shule kutumia majiko safi na ya kisasa, kupunguza matumizi ya kuni na moshi unaodhuru afya. Kutokana na teknolojia hiyo, wanafunzi watapata muda zaidi wa kujisomea badala ya kwenda kutafuta kuni, jambo litakalosaidia kulinda mazingira na kuboresha mazingira ya kazi kwa wapishi.

Kwa sasa, mpango huu unatekelezwa katika mikoa ya Dodoma, Tabora, Dar es Salaam na Kigoma, huku TEA na WFP wakiendelea kushirikiana kupanua wigo wake katika shule nyingi zaidi nchini.




*Kaimu Mkurugenzi Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi Bw. Masozi Nyirenda akitoa salamu za TEA walipokutana na Shirika la Chakula Dunia (WFP) kujadiliana jinsi wanavyoweza kushirikiana kutekeleza mpango wa chakula mashuleni.*

# 9. TEA NA TAHA WAJADILI USHIRIKIANO

Bw.Masozi Nyirenda, Kaimu Mkurugenzi wa Utafutaji Rasilimali na Usimamizi wa Miradi wa TEA, amekutana na Bw. Anthony Chamanga, Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa Chama cha Kilimo cha Bustani Tanzania (TAHA), katika kikao kazi kilicholenga kujadili mikakati ya ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili.

Ziara hiyo ilihusisha majadiliano kuhusu mbinu za kutafuta rasilimali kwa ajili ya programu za kukuza ujuzi kwa vijana na mafunzo ya amali katika sekta ya kilimo.

Ushirikiano huo unalenga kuwapatia vijana stadi za kazi zinazohitajika sokoni na kuchangia maendeleo ya uchumi nchini.




*Ujumbe kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) pamoja na uongozi wa Chama cha Kilimo Bustani Tanzania (TAHA), wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kikao maalumu cha kujadiliana mikakati ya kushirikiana.*

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**

**P.O. Box 2516, Ilazo - Dodoma.**

info@tea.or.tz www.tea.or.tz officialteatz

*"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"*